# Ndani ya Habari



**STAREHE:** Zuchu anavyowakimbiza Diamond, Harmonize UK 15

**HABARI:** Wadau wataka mabadiliko sheria wanaojaribu kujiua UK 18

## Korti yabariki faini Sh30,000 bajaji kuegeshwa isivyostahili

Daniel Mjema, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

**Moshi.** Ni kama utamaduni wa baadhi ya madereva wa pikipiki za magurudumu matatu maarufu bajaji kuegesha vyombo vyao vya moto popote, lakini bahati haikuwa ya Boniface Mtafya, kwani kosa hilo limemfikisha mahakamani alikotozwa faini ya Sh30,000.

Moshi ni miongoni mwa miji nchini Tanzania, ambayo inakabiliwa na msongamano wa bajaji kutokana na wingi wake kuliko uwezo wa barabara zake, huku madereva walio wengi wakikiuka sheria za usalama barabarani.

Madereva hao husimama popote, tena ghafla, kupakia abiria na wakati mwingine wakisimama katikati ya barabara hasa za YMCA-KCMC, Nyerere na eneo la Bora. Hali hiyo husababisha msongamano wa magari na bajaji.

Hali kama hiyo inaikumba miji mingine kama vile Dar es Salaam, Arusha, Mbeya, Mwanza, Iringa, Kigoma, Geita na mikoa mingine, ambako bajaji hutumika kama daladala na kusimama popote kupakia abiria, bila kujali watumiaji wengine wa barabara.

Mwenyekiti wa Chama cha Wamiliki na Waendesha Bajaji na Bodaboda Kilimanjaro (CWDK), Bahati Nyakiraria amepongeza hukumu iliyotolewa na mahakama, akisema adhabu za aina hiyo zinatoa fundisho kwa wengine.

"Tuna changamoto kubwa hasa baada ya faini kushuka kutoka Sh30,000 hadi Sh10,000, wapo madereva bajaji na bodaboda wanarudia makosa yaleyale waliyotozwa faini. Hili kosa la kuegesha popote kupakia abiria limekuwa sugu," amesema na kuongeza:

"Bahati nzuri hii kesi iliamuliwa na Mahakama ya Wilaya ya Moshi, mtu hakuridhika amekata rufaa Mahakama Kuu na imebariki adhabu. Nadhani kuna haja ya kuwa na data bank (kanzi data) ya wanaopatikana na hatia hata kama walilipa faini polisi."

Uendeshaji wa baadhi ya madereva bajaji na bodaboda umekuwa ukilalamikiwa karibu nchi nzima kwa kufanya makosa ya wazi ya usalama barabarani yanayochangia ajali, ambazo kati ya Januari hadi Desemba 2024 zilitokea 383 Tanzania Bara.

Kwa mujibu wa takwimu za kati ya Januari na Desemba 2024 zilizotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), ajali za pikipiki zilisababisha vifo vya watu 352, huku matukio ya uendeshaji wa vyombo hivyo kwa uzembe yalikuwa 765.



Bajaji zikiwa zimeegeshwa katika moja ya maeneo ya mjini zikisubiri abiria. **Picha na Maktaba**